TANGAZO LA SERIKALI Na. 413 la tarehe 18/09/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA ZA MWAKA ,2015

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba za Mwaka, 2015.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

“ada na Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Bidhaa” maana yake ni kitu chochote chenye thamani

kilicholetwa sokoni, mnadani au gulioni kwa lengo la kuuzwa;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chemba;

“Kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za kibiashara ndani ya eneo la Halmashauri;

“lesseni ya biashara” maana yake ni hati inayotolewa na Halmashauri kwa mfanyabiashara ambayo inamruhusu kufanya biashara katika eneo fulani ndani ya Halmashauri kwa muda maalum na kwa bidhaa zitakazoruhusiwa na Halmashauri;

“machinjio” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

“madini ya ujenzi” maana yake ni mawe, kokoto, mchanga, moramu na udongo;

“matangazo ya biashara” maana yake ni ishara, alama, maneno, maandishi yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye mabango, kuta za nyumba au vibao, kwa lengo la kutangaza biashara;

“Masoko” maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza au kununua bidhaa;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290;

“Taka” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya

Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

"Taka ngumu" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi, plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo, utengenezaji wa bustani na shughuli za uchimbaji wa madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu.

"taka za viwandani" kama ilivyotafisiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafisiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004 katika sehemu ya IX.

"Taxi" maana yake ni gari dogo linalobeba abiria wanne;

"Uchafu hatari" kama ilivyotafisiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira;

"Wakala" maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA PILI
UTOZAJI WA ADA NA USHURU

Ada, ushuru na uteuzi wa Wakala

4. (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, lesseni na huduma mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa kwenye majedwali katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika.

(3) Ada na ushuru utozwao utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika.

(4) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:

a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

b) kuwasilisha makusanyo yote anayopaswa kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

c) kumchukulia hatua za kisheria mtu, taasisi au kampuni yoyote ambayo itakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi baada ya kupata idhini ya Halmashauri.

(5) Ada na ushuru utozwao na Halmashauri utalipwa kabla ya kutolewa huduma na kabla ya mwezi unaofuata.

SEHEMU YA TATU
ADA YA USAJILI WA BIASHARA

Ada ya Usajili wa biashara

5. (1) Halmashauri itatoza ada ya usajili wa lesseni za biashara mbalimbali zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri kabla ya mfanyabiashara hajapewa idhini ya kufanya biashara kwa kulipa ada au leseni iliyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi na Sheria nyinginezo zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Ada au lesseni ya usajili wa biashara katika kifungu cha 5 (1) cha Sheria Ndogo hizi italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha na itakoma kila mwisho wa mwaka wa fedha wa Serikali.

SEHEMU YA NNE
MIPANGO MIJI

Ujenzi wa majengo na minara ya simu

6. Ni marufuku kwa mtu yeyote, taasisi au kampuni-:

a) Kujenga nyumba, jengo, kontena, minara ya simu, mabango ya matangazo ya biashara au kibanda chochote ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya bila kupata idhini au kibali cha ujenzi toka Halmashauri kwa kulipa ada stahiki inayoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi;

b) Kubadilisha matumizi ya Ardhi ya makazi, biashara, biashara na makazi kwa kuweka gereji, maegesho ya magari na matumizi mengineyo kinyume na masharti yaliyoko kwenye hatimiliki ya kiwanja au fomu ya maombi ya kiwanja yaliyoidhinishwa na

Halmashauri au Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi bila ya idhini ya Halmashauri au Wizara.

Vibanda

7. (1) Vibanda vyote vilivyojengwa kuzunguka soko na kituo cha mabasi vitakuwa ni mali ya Halmashauri.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupangisha vibanda vyake kwa wafanyabiashara watakaohitaji kufanyia biashara kama itakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote atakayepanga nyumba au kibanda kinachozunguka soko na kituo cha mabasi atatakiwa kusaini mkataba wa kupanga nyumba au kibanda hicho.

(4) Mpangaji wa nyumba au kibanda cha Halmashauri atatakiwa kulipa ada/ushuru kama itakavyopangwa na Halmashauri.

(5) Endapo mpangaji atavunja mojawapo ya masharti ya upangaji yaliyopo kwenye mkataba, Mkurugenzi atatoa notisi ya siku kumi na nne ya kusitisha upangaji wa nyumba au kibanda hicho na baada ya notisi kuisha muda wake mpangaji ataondoka kwenye kibanda au nyumba aliyokuwa amepangishwa na Halmashauri.

(6) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuingia mikataba na mtu, taasisi au kampuni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba au kibanda kuzunguka soko au stendi ya mabasi kwa makubaliano yatakayoonyeshwa kwenye mkataba.

SEHEMU YA TANO
USHURU WA MAZAO

Ushuru wa mazao

8. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao yanayolimwa kwenye eneo la Halmashauri kwa mtu, taasisi au kampuni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru wa mazao utalipwa na mnunuzi au mfanyabiashara wa mazao wakati wa kununua mazao kwenye eneo lolote la Halmashauri baada ya kupewa idhini ya kununua mazao ndani ya eneo la Halmashauri.

(3) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao yaliyohifadhiwa kwenye maghala ya mtu, taasisi au kampuni ambayo wakati wa ununuzi hayakulipiwa ushuru kama inavyoelekezwa na Sheria Ndogo hizi.

(4) Mkulima yeyote ambaye atauza mazao yake mara baada ya kuvuna au kusafirisha mazao yake toka sehemu ya mavuno kwa ajili ya kwenda kuhifadhi ili kuyauza baadae atapaswa kulipa ushuru kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo Hizi.

(5) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi wa mazao ya biashara kuwa na lesseni ya biashara pamoja na kibali cha kununulia mazao kutoka Halmashauri, kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(6) Mazao ya aina yoyote yatauzwa na kununuliwa katika masoko, magulio, minada au kwenye vituo maalum vya kununulia na kuuzia mazao vilivyotengwa na Halmashauri kama vile maghala na vituo vya ununuzi wa mazao.

(7) Mfanyabiashara yeyote atakayetaka kusafirisha mazao nje ya Halmashauri atapaswa kupata kibali cha kusafirisha mazao toka Halmashauri.

(8) Halmashauri haitatoa kibali cha kusafirisha mazao nje ya eneo la Halmashauri endapo mazao hayo yatakuwa haijalipiwa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo Hizi.

SEHEMU YA SITA
MATANGAZO YA BIASHARA

Ushuru wa matangazo ya biashara

9. (1) Kila mfanyabiashara, kampuni, shirika, Taasisi, kiwanda au mtoa huduma atakayeweka mbao za matangazo au atakayetangaza biashara au huduma yake kwa kutumia vipaza sauti, bango, michoro au maadishi ya ukutani, vipeperushi, promosheni au njia yoyote ile ya kuitangaza biashara yake atatakiwa kulipa ushuru wa matangazo kwa viwango vinavyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi;

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara, kampuni, shirika, Taasisi au kiwanda kuweka kibao cha Tangazo/Matangazo kinachoonyesha au kutambulisha biashara au eneo lake la biashara.

(3) Ni marufuku kwa mfanyabiashara, kampuni, shirika, taasisi au kiwanda kufuta au kuondoa Tangazo au bango lake la biashara kwa ajili ya kukwepa kulipa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

(4) Ni marufuku kwa mfanyabiashara, kampuni, shirika, taasisi, kiwanda au mtoa huduma yeyote

kutumia mabango au matangazo yake ya mdomo kwa nia ya kudhalilisha, kufedhehesha mtu, watu, kikundi cha watu au biashara na huduma ya mtu mwingine.

SEHEMU YA SABA
UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

10. (1) Halmashauri itatoza ada ya uchimbaji wa madini ya ujenzi kutoka kwa wachimbaji/watumiaji wa madini waliyopo katika eneo la Halmashauri na nje ya eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kusafirisha madini ya ujenzi bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(3) Mchimbaji au msafirishaji wa madini ya ujenzi ndani na nje ya eneo la Halmashauri atatakiwa kulipa ada ya uchimbaji na usafirishaji madini kama inavyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(4) Ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa wakati gari linapotoka katika eneo yanapochimbwa madini.

(5) Madini ya ujenzi yatachimbwa katika maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri.

(6) Ni wajibu wa kila mchimbaji wa madini ya ujenzi chini ya Sheria Ndogo hizi kuzingatia na kuchukua tahadhari za athari za kimazingira zitakazotokana na uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(7) Mtu yeyote atakayechimba madini katika maeneo ambayo hajatengwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA NANE
KUPIMA AFYA

Upimaji wa Afya

11. (1) Wahudumu wote wanaohudumia biashara za vyakula na vinywaji kwenye hoteli, migahawa, mashine za kusaga nafaka, baa pamoja na huduma nyingine watalazimika kupima afya pamoja na kujisajili Halmashauri kabla ya kuanza kutoa huduma.

(2) Ada ya kupima na kuthibitishwa afya kwa mhudumu italipwa kama itavyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutoa huduma kwenye hoteli, migahawa, mashine za kusaga nafaka, baa na huduma nyingine bila ya kupimwa afya na kusajiliwa na Halmashauri.

SEHEMU YA TISA
MAKOSA, ADHABU NA UKUSANYAJI WA MADENI

Makosa na adhabu

12. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:

(a) atakataa au atakwepa kulipa Ada, leseni na Ushuru anaopaswa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu, taasisi au kampuni yeyote au kundi la watu wasilipe Ada, leseni au Ushuru kwa namna yoyote;

(c) akiwa ni wakala, akishindwa kuwasilisha kiasi cha Ada au Ushuru aliokusanya kwa wakati muafaka kwa mujibu wa mkataba.

Adhabu

13. Mtu yeyote ambaye:-

a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru, leseni au ada;

b) atamshawishi mtu au kundi la watu, taasisi au kampuni wasilipe ushuru, leseni au ada;

c) atakusanya ushuru, leseni au ada bila idhini ya Halmashauri;

d) Afisa Muidhiniwa au wakala atakusanya ushuru au ada kwa kiwango ambacho ni tofauti na kilichoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

e) Atashindwa kutekeleza masharti yaliyomo katika Sheria Ndogo hizi,

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

SEHEMU YA KUMI
MASUALA MENGINEYO

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa anaweza kumtoza mtu yeyote faini nje ya Mahakama iwapo mkosaji kwa hiari yake amekubali kwa maandishi kwa kutumia fomu maalum iliyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi kulipa faini na kiasi cha ada au ushuru anachodaiwa.

Afisa Muidhiniwa

15. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote la mtu, taasisi au Kampuni kwa nia ya kukusanya ada, leseni au ushuru wa Halmashauri wakati wa saa za kazi.

Kukusanya Madeni

16. (1) Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada, leseni au ushuru kwa njia ya kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la Ada, leseni au

Ushuru kwa muda wa siku kumi na nne (14).

(2) Baada ya siku kumi na nne kuisha tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada. Uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa utakuwa halali iwapo Mkurugenzi, kwa maandishi atatoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo baada ya mwenye mali kushindwa kulipa deni analodaiwa pamoja na adhabu ndani ya kipindi cha siku saba.

(3) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza mali hizo kabla hazijaharibika, isipokuwa uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa itakuwa halali endapo Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa kwa maandishi atatoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo baada ya mwenye mali kushindwa kulipa deni analodaiwa ndani ya kipindi cha siku kumi na nne.

17. Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumfutia lesseni mtu yeyote anayekwepa ada, leseni na ushuru unaotozwa na Halmashauri.

JEDWALI 'A'
ADA YA USAJILI WA LESENI ZA BIASHARA

1)	Huduma za kibenki…….……..	TSh: 1,000, 000 kwa mwaka
2)	Uwakala wa biashara …….……	TSh. 500,000 kwa mwaka
3)	Huduma za bima……..…..	TSh. 1,000,000 kwa mwaka
4)	Huduma za posta……..…..	TSh. 500,000 kwa mwaka
5)	Huduma za umeme……..…..	TSh. 300,000 kwa mwaka
6)	Mikokoteni …… ….. …… …… …….	TSh. 2500 kwa mwaka
7)	Huduma za intaneti…… …….	TSh. 500,000 kwa mwaka
8)	Viwanda vidogo ……..	TSh. 200,000 kwa mwaka
9)	Night Clubs ……	TSh. 200,000 kwa mwaka
10)	Nyumba za kulala wageni ……	TSh. 150,000 kwa mwaka
11)	Migahawa ……	Tsh.100,000 kwa mwaka
12)	Usafirishaji wa mazao ya chakula …….	Tshs. 200,000 kwa mwaka
13)	Yadi za magari ……	Tsh. 400,000 kwa mwaka
14)	Ukandarasi ……	Tsh. 500,000 kwa mwaka

15)	Vyama vya ushirika …….	Tsh. 50,000 kwa mwaka
16)	Huduma za kitaaluma …….	Tshs. 300,000 kwa mwaka
17)	Zahanati, vituo vya afya na maabara …….	Tshs. 100,000 kwa mwaka
18)	Hospitali ……	Tsh. 150,000 kwa mwaka
19)	Maduka ya dawa muhimu za binadamu ……	Tsh. 200,000 kwa mwaka
20)	Maduka ya dawa za mifugo ……	Tshs. 200,000 kwa mwaka
21)	Maduka ya Vifaa vya ujenzi ……	Tshs. 150,000 kwa mwaka
22)	Karakana na gereji ……	Tsh. 150,000 kwa mwaka
23)	Viwanda vya mikate ……..	Tsh. 100,000 kwa mwaka
24)	Uuzaji wa mbao na samani ……..	Tsh. 100,000 kwa mwaka
25)	Duka la vitabu na stationary ……	Tsh. 100,000 kwa mwaka
26)	Mashine za kusaga ……...	Tsh. 50,000 kwa mwaka
27)	Biashara ya mifugo ……	Tsh. 100,000 kwa mwaka
28)	Mabucha ……	Tsh. 60,000 kwa mwaka
29)	Vituo vya mafuta …….	Tsh. 150,000 kwa mwaka
30)	Viosks/grosari…….	Tsh. 40,000 kwa mwaka
31)	Saluni za kike na vinyozi …….	Tsh.20,000 kwa mwaka
32)	vyumba vya chai …….	Tsh. 5,000 kwa mwaka
33)	Wauzaji wa mitumba……. …….	Tsh. 15,000 kwa mwaka
34)	Wauzaji wa spea za magari ……	Tsh.250,000 kwa mwaka
35)	Wauzaji wa spea za pikipiki ……	Tsh.80,000 kwa mwaka
36)	Wauzaji wa spea za baiskeli ……	Tsh.30,000 kwa mwaka
37)	Wauzaji wa spea za matrekta na mashine……	Tsh.60,000 kwa mwaka
38)	Mafundi umeme ……	Tsh. 200,000 kwa mwaka
39)	Kuhamisha leseni ……	Tsh. 10,000 kwa mwaka
40)	Kupewa leseni baada ya mwanzo kupotea …….	Tsh. 20,000 kwa mwaka
41)	Pikipiki ……	Tsh.20,000.00 kwa mwaka
42)	Viwanda vya alizeti ……	Tsh.200,000 kwa mwaka
43)	Maduka ya pembejeo …….	Tshs. 200,000 kwa mwaka
44)	Biashara ndogo ndogo ……..	Tshs. 50,000 kwa mwaka
45)	Biashara ambayo haijatajwa ……..	Tshs. 100,000 kwa mwaka

JEDWALI 'B'
ADA YA UNYONYAJI MAJI TAKA KWENYE MASHIMO NA HUDUMA ZA MTANDAO WA MAJI TAKA

1)	***Unyonyaji maji taka***:		
	a) Viwandani, Taasisi na Mashirika	……	Sh: 50,000.00 kwa safari
	b) Maeneo ya biashara	……	Sh: 50,000.00 kwa safari
	c) Maeneo ya makazi	……	Sh: 30,000.00 kwa safari

JEDWALI 'C'

ADA YA VIBALI MBALIMBALI NA USHURU WA MATANGAZO NA MABANGO YA BIASHARA

1)	Kibali cha muziki na disko		
	i) Onyesho la muziki wa dansi	……	Sh: 20,000.00 kwa siku
	ii) Muziki wa Disko	……	Sh: 20,000.00 kwa siku
2)	Kibali na ada ya sinema ya kwenye gari na maonyesho ya video	……	Sh: 20,000.00 kwa siku
3)	Kibali katika orodha namba 1 na 2 hapo juu kwa mtu au kampuni inayotoka nje ya wilaya	……	Sh 30,000.00 kwa siku
4)	Ada ya mikataba	……..	3% kwa kila hati ya malipo
5)	Kibali cha Maombi ya kuweka Tangazo au bango la biashara au kujenga bango la biashara	……	Sh: 20,000.00
6)	Matangazo yasiyo na taa (yasiyong'aa) kwa kila mita ya mraba	……	Sh: 8 kwa sentimita skwea kwa mwaka.
7)	Matangazo yenye taa(yanayong'aa)	……	Sh: 40.00 kwa sentimita skwea kwa mwaka.
8)	Matangazo kwa kutumia vipaza sauti	……	Sh: 10,000.00 kwa saa
9)	Kibali cha Matangazo kwa maonesho	……	Sh: 20,000.00 kwa siku
10)	Matangazo ya kubandika ***(poster)*** karatasi ya A4	……	Sh: 500.00 kwa karatasi ***(poster)*** moja.
11)	Ushuru wa malighafi za mazao ya kilimo	……..	Tshs 2,000 ya bei ya soko kwa gunia lenye uzito wa kilo 100
12)	Ushuru wa vibanda soko kuu na stendi	……..	Sh. 3,000.00 kwa mita moja ya mraba
13)	Ushuru wa kuosha magari	…….	Sh. 10,000.00 kwa mwezi
14)	Ushuru wa kuegesha magari(parking) eneo la soko	……..…..	(i) Sh. 2,000.00 kwa magari yote

	kuu na stendi na mahali kwingine kulikotengwa na Halmashauri		makubwa kwa siku
		(ii)	Sh. 1,000.00 kwa magari yote madogo kwa siku
		(iii)	SH. 500.00 kwa pikipiki
15)	Ushuru wa viwanda vya kukamua mafuta na kusaga nafaka.	……..	Sh. 5,000.00 kwa mwezi

JEDWALI "D"
ADA YA VIBALI VYA KUKATA AU KUZIBA BARABARA

1)	Kukata barabara ya lami	……	Sh: 200,000 kwa mita
2)	Kukata barabara ya kifusi	……	Sh: 5,000 kwa mita
3)	Kukata barabara ya udongo	……	Sh: 2,000 kwa mita
4)	Kukata pembezoni mwa barabara kusikosakafiwa mjini	……	Sh: 2,000 kwa mita
5)	Kufunga barabara kwa ajili ya sherehe na shughuli nyingine isipokuwa msiba ambapo kibali kitatolewa bure	……	Sh: 15,000 kwa siku

JEDWALI "E"
USHURU WA MADINI YA UJENZI

1)	Tani 1 – 3½	……	Sh: 2,000.00 kwa safari
2)	Tani 4 – 7	……	Sh: 3,000.00 kwa safari
3)	Tani 8 na kuendelea	……	Sh: 5,000.00 kwa safari

JEDWALI "F"
USHURU WA MACHINJIO

	Aina ya mnyama		**Ushuru**
1)	Ng'ombe	-----	Sh: 10,000.00 kwa kila ng'ombe atakayechinjwa
2)	Mbuzi/kondoo	-----	Sh: 5,000.00 kwa mbuzi/kondoo atakayechinjwa
3)	Nguruwe	-----	Sh: 5,000.00 kwa kila nguruwe atakayechinjwa

JEDWALI "G"
ADA YA HUDUMA ZA ARDHI

A. Ada ya maombi ya mabadiliko ya matumizi ya Ardhi

a) Makazi kuwa biashara ……Tshs. 20,000/=

b) Biashara kuwa Viwanda …… Tshs. 25,000/=

c) Biashara kuwa makazi …….. Tshs. 20,000/=

d) Viwanda/Biashara kuwa kituo cha mafuta …….…….. Tshs. 30,000/=

e) Kugawanya kiwanja au shamba ……..… Tshs. 20,000/=

B. Ada ya maombi ya idhini ya ujenzi

i. Nyumba za makazi …….. Tshs. 20,000/=

ii. Nyumba za biashara ……... Tshs. 30,000/=

iii. Nyumba za biashara na makazi ……..... Tshs. 40,000/=

iv. Ofisi binafsi, shule binafsi, hospitali binafsi……Tshs. 200,000/=

v. Ghala/Bohari …….Tshs. 200,000/=

vi. Majengo mengine ambayo hajatajwa ……..…. Tshs. 20,000/=

vii. Minara ya simu …….. Tshs. 300,000/=

viii. Ghorofa zaidi ya moja ……. Tshs. 200,000/=

ix. Nyumba za biashara (Nyumba za kulala wageni,
Hoteli, Maduka, Malls ……. Tshs. 100,000/=

x. Kituo cha mafuta …… Tshs.500,000/=

f) Kibali cha kuweka kontena la biashara …….…… Tshs. 40,000/=

g) Kibali cha kuweka kioski …… Tshs. 20,000/=

h) Kibali cha kibanda cha saloon …… Tshs. 20,000/=

i) Kibali cha kibanda cha mitumba …….….. Tshs. 30,000/=

j) Kibali cha pampu ya mafuta ya taa ……..... Tshs. 50,000/=

k) Kibali cha kufyatua tofali …… Tshs. 30,000/=

l) Kibali cha kuanzisha vyoo vya kulipia ……..……. Tshs. 30,000/=

m) Kibali cha kujenga kiwanda ……. Tsh. 200,00/=
n) Kibali chochote ambacho hakijatajwa…….……. Tsh. 50,000/=

B. Ada ya Kuchangia upimaji Ardhi wa jumla

a) Kiwanja kidogo (High Density) ……..…… Tshs. 200,000/=

b) Kiwanja cha Kati (Medium Density) …….……. Tshs. 300,000/=

c) Kiwanja kikbwa (Low Density) ……..…… Tshs. 400,000/=

d) Kiwanja kikubwa (Super Low Density) …….…….. Tshs. 500,000/=

JEDWALI "H"
KODI YA PANGO, MAJENGO NA VIBANDA VYA HALMASHAURI

S/N	Aina ya Jengo	Kodi ya pango	Muda
1	Vibanda ndani ya soko	Tshs. 30,000/=	Kwa mwezi
2	Vibanda nje ya soko	Tshs. 25,000/=	Kwa mwezi
3	Vibanda ndani ya stendi	Tshs. 30,000/=	Kwa mwezi
4	Vibanda nje ya stendi	Tshs. 25,000/=	Kwa mwezi
5	Nyumba ya makazi ya Halmashauri a) Nyumba kubwa b) Nyumba ndogo	 10% ya mshahara wa mtumishi 7% ya mshahara wa mtumishi	 Kwa Mwezi Kwa Mwezi
6	Kodi ya pango kwa ajili ya minara ya simu iliyosimikwa kwenye maeneo ya Halmashauri	Bei ya soko la ardhi	Kwa mwaka

JEDWALI "I"
USHURU WA MAZAO YA KILIMO NA BIASHARA

S/N	**Aina ya Zao**	**Kiwango cha Ushuru**
1	Mahindi	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
2	Mtama	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
3	Uwele	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
4	Maharagwe	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
5	Mchele	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
6	Alizeti	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
7	Ufuta	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
8	Karanga	3% ya bei ya soko kwa kila gunia

9	Soya	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
10	choroko	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
11	Miwa	Tshs.1,500 kwa tani moja ya gari
12	Ulezi	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
13	Kunde	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
14	Vitunguu	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
15	Mashudu	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
15	Mazao mengine ambayo hayajatajwa	3% ya bei ya soko kwa kila gunia

JEDWALI "J"
ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

S/N	Aina ya Mnyama	Kiasi	Idadi
1	Ng'ombe	Tshs. 5,000/=	Kwa ng'ombe
2	Mbuzi/Kondoo	Tshs. 2,500/=	Kwa mbuzi/Kondoo
3	Nguruwe	Tshs. 2,500/=	Kwa nguruwe
4	Mnyama mwingine asiyetajwa	Tshs. 1,000/=	Kwa mnyama

JEDWALI "K"
USHURU WA NGOZI

S/N	Aina ya Ngozi	Ushuru	Idadi
1	Ngozi ya Ng'ombe	Tshs. 1000/=	Kwa kipande
2	Ngozi ya Mbuzi	Tshs. 500/=	Kwa kipande
3	Ngozi ya Kondoo	Tshs. 500/=	

JEDWALI "L"
ADA YA KUPIMA AFYA

S/N	Aina ya Ada	Kiasi	Muda
1	Ada ya kupima Afya	Tshs. 5,000/=	Kila baada ya miezi minne
2	Ada ya ukaguzi wa kiafya kwenye nyumba za biashara	Tshs. 5,000/=	Kwa Mwezi
3	Ada ya ukaguzi wa kiafya kwenye nyumba za makazi	Tsh. 2,000/=	Kwa mwezi

JEDWALI "M"
USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

S/N	Aina ya zao	Kiasi	Kipimo
1	Mbao laini	Tshs. 500/=	Kila ubao
2	Mbao ngumu	Tsh. 600/=	Kila ubao
3	Mkaa	Tshs. 500/	Kwa gunia
4	Kuni	Tshs. 100/=	Kwa kila mzigo

5	Boriti/Nguzo	Tshs.200/=	Kwa kila boriti
6	Magogo	Tshs. 1,000	Kwa kila gogo
7	Fagio	Tshs.50/=	Kwa kila ufagio
8	Asali/Nta	Tshs. 500/=	Kwa kilo moja
9	Fito	Tshs.100/=	Kwa fito
10	Nyungo	Tshs. 100/=	Kwa kila ungo
11	Mazao mengine yasiyotajwa	Tshs. 500/=	Kila mmoja

JEDWALI (N)
FORM NA. 1

MAOMBI YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO KATIKA MASOKO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

(SEHEMU "A")
(Ijazwe na mwombaji)

1. Jina la Mnunuzi ……..
2. Jina la kampuni/shirika, n.k …….
3. Anwani, S.L.P ……MJI …….. SIMU …….
4. Mahali ofisi ilipo ……..
5. Mahali anapoishi mwombaji …….
6. Namba ya lesseni ya ununuzi wa mazao ……..
7. Aina ya mazao anayotaka kununua ……..
8. Kiasi cha mazao anachotaka kununua ……
9. Masoko/Sehemu atakaponunulia mazao ……..
10. Maghala yalipo : Mji/Kijiji ……Mtaa ……Kiwanja No……
11. Jina la Ghala/Maghala ……..

Nathibitisha kuwa maelezo niliyoyatoa hapo juu ni sahihi na ni kweli na nitawajibika kwa maelezo ambayo nimeyatoa nikijua kuwa siyo ya kweli.
Jina la Mwombaji ……
Saini ya Mwombaji ……
Tarehe
…….
Muhuri wa Ofisi …….

(SEHEMU "B")
(Ijazwe na Halmashauri)

KIBALI

1. Mwombaji aliyetajwa hapo juu amepewa/hajapewa kibali cha kununua mazao kwa sababu……
2. Mwombaji amelipa/atalipa ushuru wa Tsh…… kwa kiasi cha mazao gunia/tani …… ambayo ni ……
   Kwa msimu wa ununuzi wa mwaka ……..

Jina la Afisa
……
Cheo
……..
Muhuri
……..
Tarehe
……..

JEDWALI (O)
FOMU NA.2
FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya Kifungu Na.14 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi……wa S.L.P…… ninaefanya biashara ya …… katika eneo la …… lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, nakiri kuwa leo tarehe ……nilikiuka kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba za mwaka 2015. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi.

Jina……..……
Saini…..…….
Tarehe …….

Mbele yangu;
Jina…….
Saini ……
Wadhifa ……
Tarehe ……..

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilibandikwa katika sheria ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba uliofanyika tarehe 25 Mwezi 04 Mwaka 2014, Muhtasari Na. 11/2013/2014 mbele ya:

DKT. WILLIAM D. MAFWERE
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Chemba

MHESHIMIWA RAJABU
Mwenyekiti wa Halmashauri ya
Wilaya ya Chemba

NAKUBALI

Dodoma,
8 Julai, 2015

MIZENGO PETER PINDA (MB),
Waziri Mkuu